TOLEO NO.66

# Khilafah

RABIUL AWWAL 1447 HIJIRIA — SEPTEMBA 2025 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh

NDIO SULUHISHO

## NDOTO YA DIRA YA MAENDELEO YA TANZANIA 2050




Julai 17, 2025, Tanzania ilizindua Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma, Dira ambayo iliitaja kuwa ni hatua ya kihistoria kwa mabadiliko ya kijamii na kiuchumi nchini katika kipindi cha miaka 25 ijayo.

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 'Tanzania Development Vsion 2050', ambayo eti inataka kuigeuza Tanzania kuwa jamii yenye kipato cha juu, imara, yenye kutenda haki, na jumuishi ifikapo mwaka 2050, ni mrithi wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 'Tanzania Development Vision 2025' inayomaliza muda wake, ambayo iliundwa mwaka 1999 ikiwa na malengo kadhaa — miongoni mwao ni kufikia maisha bora kwa wananchi wote. Kwa bahati mbaya, malengo yote yaliyotajwa katika dira ya 2025 hayakufaulu na badala yake kumekuwa na matatizo zaidi kwa watu maskini wasiojiweza.

Suala la kufikia maisha bora kwa wananchi wote lilikuwa kauli mbiu tupu iliyoleta matokeo tofauti na kinyume yake. Mwaka 2000, masikini waliokuwa chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi ilikuwa 35.7%, wakati mwaka 2024, ilipanda hadi 43% kulingana na

**Inaendelea Uk. 3**

## MTUME (SAAW) ALIKUWA NABII NA MTAWALA



Wakati tukiwa katika mwezi aliozaliwa kiongozi wetu mtukufu Mtume SAAW lazima kufafanua nafasi yake kwetu na kwa ulimwengu mzima ambayo ni Utume na utawala.

Kwa bahati mbaya na kwa masikitiko makubwa baada ya kipindi kirefu cha mporomoko wa fikra na ufahamu sahihi juu ya Uislamu, kumekuwa na kampeni kubwa ya kuipigiwa debe fikra ya kikafiri kisekula ya kutenganisha dini na dola iliyopelekea kuipotosha nafasi ya Mtume SAAW.

Katika hilo kuna baadhi kwa lengo la kuupotosha Umma hudai kuwa Mtume (SAAW) hakuwa na dola na hivyo hakuwa mtawala. Kwa kuangalia sira ya Mtume (SAAW) na

**Inaendelea Uk. 6**

## Yaliyomo :

- Maulidi yatupe msukumo wa kubeba majukumu sio sherehe tu..uk.2
- Mikataba miwili katika mkataba mmoja…………………………..uk.4
- Mtume (saaw) ni Rehma kwa walimwengu wote …………………..uk.5
- Dini mseto haina nafasi katika Uislamu……………………..…...uk.8



## MAULIDI YATUPE MSUKUMO WA KUBEBA MAJUKUMU SIO SHEREHE TU

Tukiwa katika mwezi wa Rabi-ul Awal, mwezi aliozaliwa kigezo chetu, kiongozi wetu na Mtume wetu mtukufu Muhammad SAAW ambapo Umma wetu mashariki na magharibi hutenda amali mbali mbali hususan maulidi kuyakumbuka mazazi yake.

Pamoja na amali hizo mbali mbali kama mihadhara, makongamano,khutba, bayan, maulidi nk. lazima Umma wetu utanue upeo mpana katika kuyakumbuka mazazi hayo

Upeo na ufahamu huo utokane na lengo na jukumu kubwa la kuletwa kiongozi wetu huyo na Muumba wetu na sio kuzifanya hafla hizo kuwa ndio lengo lenyewe.

Kazi na jukumu kubwa la Mtume SAAW lilikuwa ni kubalighisha nuru ya Uislamu ipasavyo, kuutangaza kwa ulimwengu na kuutawalisha, ili uwe mfumo ulio juu ya mifumo mengine yote.

Mtume SAAW alilibeba jukumu hilo kwa uaminifu usio na mfano, kwa muhanga mkubwa, na kwa jitihada yake yote licha ya vizingiti mbalimbali vya makafiri, lakini hakurudi nyuma wala kutetereka akaendelea kulibeba jukumu hilo mpaka siku yake ya mwisho kilipomfika kifo.

Vivo hivyo, masahaba na makhalifa baada yake walishika mikoba yake na kupasiana kijiti cha kuilinda, kuihifadhi na kuitwalisha aqida ya Kiislamu kwa ikhlasi, ujasiri mkubwa na ukweli hadi kufikia kiwango cha Uislamu kutawala sehemu kubwa ya

dunia na nuru hiyo ya Uislamu kutufikia sisi.

Leo Mtume (SAAW) hayupo lakini risala na mafundisho yake yapo hai, licha ya kukabiliwa na changamoto kubwa ya kukosa dola ( Khilafah) kuyatekeleza katika kiwango cha kimfumo. Kwa hivyo, nyakati kama hizi za mazazi ya Mtume SAAW Umma wetu usibaki katika kushughulishwa na amali za kumbukumbu za uzawa wake tu, bila ya kufujifungamanisha na majukumu tuliyoachoiwa na y eye Mtume SAAW ambaye kwetu ni kigezo thabiti.

Mashaka yanayopitia Umma wetu katika mauaji ya kijidola bandia cha mayahudi na washirika wake ndani ya Gaza,Yemen, vita ndani ya Sudan, mateso ndani ya Kashmiri, Turkistan Mashariki, Mymanar, dhiki za kiuchumi, umaskini, ujinga nk ni matokeo ya kuwa risala ya Mtume saaw haifanyi kazi kiutawala katika maisha yetu.

Basi shime enyi Umma wetu, masiku haya ya kumbukumbu ya uzawa wa Mtume SAAW yaturejeshe katika mwelekeo sahihi wa kuyabeba ipasavyo majukumu

SAAW ili kuukomboa Umma wetu na ulimwengu kutokana na hali duni, idhilali na mdororo kwenda katika hali ya faraja na ufanisi katika dunia hii na maisha yajayo akhera.

Mhariri

**01 Rabiul Awwal 1447 Hijria**

**Septemba 2025 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

#MazaziYaMtumeUkomboziKwaGaza

## Ndoto ya dira ya maendeleo ya Tanzania 2050... *Kutoka uk .1*




Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia mtawalia. Bila kusahau kuwepo kwa mambo mengine mengi ya kijamii na kiuchumi ambayo yalikwamisha shughuli za kiuchumi kwa wananchi, kama vile kutoweka kwa lazima na utekaji nyara haswa kutoka mwaka 2017.

Kama ilivyokuwa kwa mtangulizi wake, Dira ya 2050 inatarajiwa itakuwa sawa na kushindwa kama mtangulizi wake- itaishia kuwa ndoto ya mchana.

Kumekuwa na mipango mingi, mikakati, dira n.k tangu Tanzania ilipopata uhuru wake mwaka 1961, kama vile Mpango wa Maendeleo (1964-1981), Mpango wa Maendeleo (1981-1994), na kadhalika. Hakuna yeyote iliyofikia malengo yake bali kinyume chake, mipango yote, mkakati yote na Dira vimekuwa si lolote si chochote bali ni mipango ya kikoloni kutoka kwa wakoloni wa magharibi inayolenga unyonyaji wa rasilimali za nchi maskini na sio kuziendeleza.

Kwa mfano, Dira ya 2025, iliwekwa kufikia malengo ya kikoloni ya kimataifa yanayoitwa 'Malengo ya Maendeleo ya Milenia', wakati Dira hii mpya ya 2050 inatazamiwa kufikia malengo mapya ya kikoloni yaani 'Malengo ya Maendeleo Endelevu'

Nchi zinazoendelea kama vile Tanzania, licha ya kuwa na rasilimali nyingi, haziwezi kamwe kujiendeleza kupitia mipango hii iliyobuniwa na wakoloni na inayoitwa 'dira', kama tunavyoshuhudia kwa miaka mingi.

Kinachohitajika kwa mataifa machanga yanayoendelea ni kufanya mabadiliko makubwa ya kimfumo kutoka katika mfumo muovu wa Ubepari hadi mfumo wa haki na uadilifu wa Uislamu. Chini ya Dola yake ya kiulimwengu ya Khilafah, nchi masikini, zinazokandamizwa na zinazonyonywa, zitakombolewa kutoka katika minyororo ya ukoloni wa kimagharibi na unyonyaji, na badala yake zitapewa mipango na dira za kiuchumi zenye uadilifu, zenye uhalisia, na madhubuti ambazo zinalenga haki na ustawi kwa wote.

**Imeandkiwa na Said Bitomwa**
**Mjumbe wa Afisi ya Habari Hizb ut Tahrir Tanzania**

******




## MATUKIO YA TARIIKH MWEZI WA RABI-UL-AWWAL

1. Uzawa wa Mtume SAAW Bwana wa Mitume Muhammad bin Abdillah SAAW alizaliwa katika mtaa wa Banu Hashim (Mwaka wa ndovu)
2. Ndoa ya Mtume SAAW na mama Khadija bint Khuwaylid. Huyu ndie mke wa kwanza wa Mtume SAAW.
3. Kutangazwa Ufaradhi wa Swala Tano. Ibada hii ilitangazwa rasmi ndani ya Mwaka wa 1 Hijria

4.Ghazwatu Buwat. Mtume SAAW aliongoza kikosi cha watu 200 ili kudhoofisha uchumi wa makureish na kuandaa mazingira ya vita. Bendera ya vita ilibebwa na Saad bin Abi Waqas, na uongozi wa dola Madina ulikabidhiwa kwa Saad bin Muadh kwa muda. (mwaka wa 2AH kabla ya Vita vya Badr)

5.Ghazwatu Swafwan. Mtume SAAW alitoka na kikosi cha askari 70 kumfukuza Kurz bin Jabir Al-Fihriy na wenzake kufuatia mashambulizi yao katika malisho na uporaji wa wanyama. Bendera ya vita ilibebwa na Ali bin Abi Twalib ra.Uongozi wa dola ulikabidhiwa kwa Zaid bin Harithah. (Mwaka wa 2AH. Kabla ya vita vya Badr)
6.Kuuliwa kwa Kaab bin Ashraf. Mtume SAAW aliamuru kuuwawa kwa Yahudi muovu Kaab

**Inaendelea uk. 7**

## MIKATABA MIWILI KATIKA MKATABA MMOJA

**Swali:**
Mtu anataka kununua gari kwa njia ya Halal, lakini akaelekezwa kuwa kuna kampuni fulani inayokodisha gari kwa muda mrefu ambayo pia kuna uwezekano wa kuimiliki baada ya kuisha kwa mkataba wa kukodisha. Ikimaanisha kuwa hii ni mikataba miwili. Je inaruhusiwa?

**Jibu:**
Mikataba katika Uislamu ni mepesi na iko wazi; na mkataba mmoja hauchanganywi na mktaba mwengine. Kinyume na hali ilivyo katika sheria za kibinadamu.
Mtume (saw) ameharamisha kufungwa kwa mikataba miwili kupitia mkataba mmoja: Mfano mtu kusema nakuuzia nyumba yangu kwa sharti ununue na nyumba yangu nyengine au nakuuzia nyumba yangu na wewe uniuzie nyumba yako. Hilo haliruhusiwi kwa kuwa ni mikataba miwili iliyojumuishwa katika mkataba mmoja, kwani ukisema **nakuuzia nyumba yangu** ni mkataba wa kwanza na ukisema **kwa sharti nami uniuzie nyumba yako** ni mkataba wa pili na yote imejumuishwa katika mkataba mmoja. Imesimuliwa kutoka kwa Ahmad Abdul Rahman bin Abdullah bin Masood, kutoka kwa babake, alisema:
***"Mtume (saw) ameharamisha mikataba miwili ndani ya mkataba mmoja"***
Hivyo kutokana na suali lako, kuna mkataba wa ukodishaji wa gari kwa muda fulani kisha baada ya muda huo unakuwa ni mkataba wa uuzaji wa gari. Makubaliano hayo mawili ya ukodishaji na



uuzaji wa gari kati ya mmiliki wa gari na mkodishaji wa gari yako ndani ya mkataba mmoja. Hivyo kwa mujibu wa Hadith hiyo hairuhusiwi.

Ama ungetaka suluhisho, ungelikubaliana na mwenye gari akuuzie gari hilo kwa mkopo, umpe kima cha kuanzia na kima kitakachobakia ukamlipa kidogo kidogo mpaka utakapokamilisha bei muliokubaliana hapo awali, na kwa hali hiyo gari hilo litakuwa ni lako kwa mujibu wa mkataba wa mauziano muliokubaliana awali. Mkataba huu ni mkataba wa mauziano kwa mkopo na unaruhusiwa **lakini kwa sharti ya kuwa bei ya uuzaji iwekwe wazi tangu mwanzo wa mkataba ima ni kwa malipo ya mkono kwa mkono au ni malipo ya mkopo wa kulipa kidogo kidogo, na mkataba wa mauziano hufungwa kwa makubaliano ya wahusika.**
Kwa hivyo ikiwa wote wamekubaliana juu ya bei fulani, na muuzaji akamuuzia mnununuzi kwa bei ya mkono kwa mkono (cash) na mnunuzi akakubali au akamuuzia kwa bei ya mkopo na mnunuzi akakubali, hili **linaruhusiwa** maanake ni kujadiliana juu ya bei ya uuzaji sio uuzaji. Kujadiliana kumeruhusiwa. Imesimuliwa na Anas bin Malik kuwa Mtume (saw) aliuza blanketi na bakuli la kunywea maji akasema: *"Nani atakaye nunua blanketi na bakuli la kunywia maji?" Bwana mmoja akasema: Nitazinunua kwa Dirham moja. Mtume (saw) akasema: "Nani atakayetoa zaidi ya Dirham? Nani atakayetoa zaidi ya Diraham? Bwana mmoja akakubali kumpa Dirham mbili, Mtume (saw) akamuuzia.*

**Vilevile, wengi wa wanavyuoni wamesema ya kwamba inaruhusiwa kuuza kitu kwa mkopo kwa bei ya juu kuliko bei yake ya mkono kwa mkono (cash). Imesimuliwa ya kwamba Tawoos, Al-Hakam na Hammad walisema kuwa hakuna makosa ikisemwa: Nakuuzia kwa bei kadhaa ikiwa ni mkono kwa mkono na kwa bei kadhaa ikiwa ni kwa mkopo, naye atachagua moja kati yao. Imam Ali (ra) alisema: Yoyote mwenye kuuza kwa bei mbili; moja ya mkono kwa mkono na nyengine ya mkopo, basi na ataje mojawapo kabla ya kufunga mkataba.**

**Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye Hekima.**

Ndugu yenu Ata bin Khalil Abu Rashta.

Amiri wa Hizb ut Tahrir

********

**USIKOSE KUSOMA JARIDA LAKO LA KHLAFAH KILA MWEZI**

## MTUME (SAAW) NI REHMA KWA WALIMWENGU WOTE

Tumo ndani ya mwezi wa Rabi-ul Awwal, mwezi aliozaliwa Mkombozi wa ulimwengu, Mtume Muhammad SAAW ambae alikuwa ni Rasul na pia mtawala aliyekuja kusimamia maisha ya wanadamu kwa nidhamu maalumu kukabiliana na matatizo yote ya mwanadamu.

Wanafikra mbalimbali wasio Waislamu hususan wa kimagharibi wanakiri juu ya utukufu wa haiba ya Mtume SAAW. Lakini kwa upana wake, Utume wake unasadikishwa sio tu na hoja za kiwahyi bali hata kwa hoja za kiakili. Yeye Muhammad SAAW ndie pekee aliyekuwa mpokeaji wa wahyi wa kitabu cha Quran kilichoteremshwa kwa lugha fasaha ya kiarabu. Kitabu walichoshindwa waarabu wenyewe kutoa mithili yake. Kushindwa huko ni hoja ya kukinaisha kiakili kuwa Quran Tukufu haikutungwa na waarabu, wala haikutungwa na Mtume SAAW. Kwa kuwa nae ni miongoni mwa waarabu. Bali ni wahyi kutoka kwa Allah Ta'ala. Na hii ni ithibati toshelezi kabisa kuwa aliyepokea kitabu hicho ni Mtume wa Allah. Kwa kuwa anaepokea wahyi huwa ni Mtume na sio mwengineo.

Mtume SAAW alitumilizwa katika zama zilizosheheni kila aina ya uovu, upotofu na ufisadi katika kila kipengee cha maisha ya mwanadamu kama hali ilivyo leo. Ulimwengu ulikuwa umegubikwa na maharibiko na madhila



makubwa ya kijamii kama kuuwa watoto wa kike, kudharau wanyonge, ubaguzi wa rangi na kikabila nk. Dhulma za kuchumi kama riba, kupunja vipimo, kuporwa misafara ya kibiashara nk. Na kwa upande wa kisiasa, katika maeneo machache mamlaka za maamuzi yalihodhiwa na baadhi ya makabila au koo fulani, ilhali sehemu kubwa ya watawala hao walikuwa wakala au vibaraka wa madola ya Roma na Fursi yaliyokuwa ndio madola makubwa kwa wakati ule. Kama ilivyouhodhi ulimwengu leo Marekani baada ya kuanguka dola la Kisovieti.

Pamoja na ufisadi wote huo na kuwepo madola makubwa yenye nguvu na mabavu, bado ujio wa Mtume SAAW ulitangazwa kuwa ni Rehma kwa walimwengu. Tena ni Rehma inayondelea mpaka Siku ya Mwisho. Kwa kuwa Muhammad SAAW ni Mtume wa mwisho, tangazo hili lilikuwa na makusudio mawili makubwa:

**Kwanza,** kila pasipotawaliwa na muongozo wa Mtume Muhammad SAAW daima patakuwa pamegubikwa na hali ya uovu na ufisadi. Hata kama dola inayotawala ni dola kubwa. Kwa kuwa kinyume cha Rehma ni laana, balaa, tabu na mashaka.

**Pili,** ili wanadamu waokoke na kusalimika kikweli hawana budi kukubali na kufuata muongozo ambao ni Rehma kwa walimwengu wote. Au walau kuwa chini ya kivuli cha muongozo wa Rehma hiyo.

Mtume SAAW ni Rehma 'maalum' kwa Waislamu. Kwa kuwa wao watamuamini na kufuata aliyotumilizwa nayo na kuyafanyia kazi yakiwa ni masuluhisho ya matatizo yote ya mwanadamu. Waumini hao watapata utulivu katika hii dunia, na akhera watakuwa ni wenye kufaulu kikweli. Kwa upande mwengine, Mtume SAAW ni Rehma kwa walimwengu wote kiujumla wakiwemo hata wasiokuwa Waislamu. Japo kwamba wao hawatomuamini wala hawatolazimishwa kumuamini, lakini katika hii dunia watapata Rehma zake kwa kutawaliwa chini ya kivuli cha dola inayofuata muongozo wa Mtume SAAW. Watashuhudia kheri, uadilifu, kuamiliwa kwa insafu na wema chini ya mfumo wa Uislamu na Waislamu. Kama inavyoshuhudiwa na historia inayong'ara katika zama za Mtume SAAW na makhalifa baada yake. Na vivo hivyo yatashuhudiwa hayo mara itakaporudi tena dola ya Khilafah kwa mara ya pili, kwa idhini ya Allah Taala.

Ni jambo nyeti na lazima katika mwezi huu aliozaliwa Mtume SAAW kwa Waumini kutambua dhima kubwa waliyonayo na kuieneza Rehma ya Mtume SAAW kifikra na kiusimamizi. Na kwa wasiokuwa Waislamu hususan waadilifu miongoni mwa 'wanafikra makini'

**Inaendelea uk ...7**

*nusus* katika sharia zinaonyesha wazi bila ya tembe ya shaka kuwa Mtume (SAAW) mbali ya U-nabii wake lakini pia alikuwa ni Mtawala aliyetawala na kuendesha dola.

Mtume (SAAW) alikuwa ni kiongozi/mtawala wa wazi kabisa tokea kupewa kiapo yaani Baia'h ya Pili ya Aqaba. Katika Sira ya Ibn Hisham tunaona kuwa Mtume (SAAW) alipokutana na watu wa makabila ya Aus na Khazraj walipokuja Makkah alisema kuwaambia:

*"Nitaingia katika makubaliano ya kiapo pamoja nanyi muda wa kwamba mutanihifadhi kama mnavyowahifadhi wanawake wenu na watoto wenu".* Baraa (ra) akanyoosha mkono wake ili ambayiishe kwa hayo, akasema: ***"Tumekubayiisha ewe Mtume wa Allah, wallahi sisi ni watu wa vita na watu wa silaha na tumezirithi kutoka kwa mababu na mababu".*** **Na kabla Baraa (ra) hajamaliza maneno yake Abu Haitham bin Tayhan akamkatiza kwa kusema:** ***Ewe Mtume wa Allah kati yetu na watu (yaani Mayahudi ) kuna mkataba na sisi tutauvunja , na iwapo tutafanya hilo na kisha Allah akakupa ushindi utarudi kwa watu wako na kutuacha?*** Mtume (saw) akatabasamu na akasema ***"Bali damu yenu ni damu yangu na kitukufu chenu ni kitukufu kwangu, mimi ni katika nyinyi na nyinyi ni katika mimi, tutapigana na yeyote mutakaepigana nae na nitaweka amani na Yule mlioweka nae amani."*** Baadae wakatoa baia'h kwa Mtume (SAAW) na kutamka ***"Tumembayiisha Mtume (saw) juu ya kusikiza na kutii katika mazito yetu na mepesi yetu na yanayotuchangamsha na yanayotuchukiza na tusiwe wenye kujipendelea na wala tusizozane kuhusu utawala na wanaohusika"***. Kisha Mtume(SAAW) akasema: *"Nitoleeni watu kumi na mbili kati yenu ili wawe ni wasimamizi juu ya watu wao".*

Jamii ya Madina haikuwa ni mkusanyiko holela wa Waislamu, bali ilikuwa na muundo na fungamano maalum. Mtume (SAAW) tangu alipoingia Madina aliweza kuunda mfumo wa kisiasa na kuweka taratibu, kanuni, udhibiti na utii katika jamii. Huku akifanya kazi zilizo chini yake akiwa ni mtawala. Mtume (SAAW) alisaini mikataba pamoja na Mayahudi,, Banu Dhamrah na Banu Madlaj. Baadae mikataba ilifungwa pamoja na Makureshi na watu wa Ayla, Al-Jarba na Uzra. Baadhi ya nukta muhimu katika moja ya mikataba inasomeka hivi:

1. Marafiki wa Mayahudi ni kama wao. Asitoke yeyote nje ya Madina isipokuwa kwa idhini ya Muhammad

2. Yathrib ni tukufu kwa watu wa mkataba.

3. Iwapo mvutano au ugomvi utatokea na ikahofiwa uharibifu basi marudio yake ni kwa Allah Azzah wa Jallah na kwa Mtume wake SAAW.

4. Makureshi na wasaidizi wao wasipewe hifadhi.

Mtume (saw) akiwa ni kiongozi mtawala wa dola, aliunda muundo maalum wa dola (structure of the state) unaojumuisha kuwa na wasaidizi katika utawala na masuala ya kiutendaji. Walikuwepo viongozi kama Amir wa jihadi, Ma-wali (Magavana), Ma-kadhi, Majlis Ummah (Shura) nk. Imepokewa na Tirmidhi na Hakim kutoka kwa Abi Said Al Khudhri amesema: Amesema Mtume (SAAW): *"Mawaziri (wasaidizi) wangu wawili kutoka mbinguni ni Jibril na Mikail, na katika ardhi ni Abubakar na Umar".*

Mtume (SAAW alisimamia jeshi na kuteuwa viongozi/ maamiri wa Jihad. Alimteuwa Abu Salama Ibn Abdil Asad (ra) kuwa ni kamanda wa kikosi cha watu 150 na alimkabidhi bendera. Katika vita vya Mu'tah alimchagua Zaid bin Harithah kuwa kiongozi, na akawateuwa viongozi baada yake iwapo atauawa.

Aidha, Mtume SAAW aliwahi kumteuwa Usama bin Zaid katika uongozi kama huo. Imepokewa na Muslim kutoka kwa Suleiman bin Buraid kutoka kwa baba yake:

***"Mtume (SAAW alipokuwa akimteuwa mtu kuwa Amiri wa jeshi au misafara alimuusia uchamungu kwanza yeye mwenyewe, kisha Waislamu wote kwa ujumla kufanya mambo ya kheri"***

Dola ya Kiislamu ilipotanuka, Mtume (SAAW) akiwa ni mtawala mweledi (stateman) alichagua ma-wali na ma-a'mil katika kila wilaya na miji ili wasimamie uendeshaji wa mambo ya watu na kutatua matatizo yao. Alimchagua Utba bin Usayd (ra) kuwa wali wa Makkah, Muadh bin Jabal kuwa wali wa al-Janad nk.

Mtume (SAAW kutokana na mamlaka yake ya utawala alichaguwa ma-kadhi kwa lengo la kutowa hukumu **Inaendelea uk … 7**

## Nabii na Mtawala ... *Kutoka uk .6*

kwa njia ya kulazimisha ili itatuke mizozo baina ya watu. Mfano, alimteuwa Ali (ra) kuwa kadhi wa Yemen na kumuelekeza, akasema SAW:

***"Wakikujia watu wawili ili uwahukumu basi usimhukumu wa mwanzo mpaka umsikilize wa pili ndipo utakapojua vipi utatoa hukumu"***

**(Tirmidhi na Ahmad)**

Ili upatikane ufanisi mzuri katika uendeshaji na kuhudumiwa raia vizuri zaidi, Mtume (SAAW) aliunda baraza la ushauri (Shura). Alikuwa akitaka ushauri kwa watu weledi wakiwemo Muhajirun na Ansar wanaowakilisha watu wao. Na katika watu maalum katika Masahaba wake kuwafanya makhsusi kwa ushauri kama Abubakar, Umar,Hamza, Ali, Salman Alfarisy, Hudhaifa nk.

Kwa kuzingatia haya ambayo ni baadhi ya aliyoyatekeleza Mtume (SAAW) ikiwemo kufunga mikataba baina ya tawala, kuweka katiba na kanuni za kuendesha mambo ya serikali, kuunda jeshi na kulituma kupinduwa tawala nyengine, kuweka magavana (wali) katika kila wilaya za dola, kuteua na kutuma mabalozi nk. inaonyesha wazi kuwa Mtume SAAW alikuwa ni mtawala. Lakini kuwa kwake mtawala hakukumuondoshea cheo cha Utume wake. Hivyo Mtume SAAW alikuwa ni Mtume na pia Mtawala.

*******

## Rehma Kwa ... kutoka uk 5

ambao wapo wengi, ni muhimu kwao kutafiti kwa uadilifu mfumo wa Mtume SAAW bila ya kuathiriwa na uadui na propaganda na uzushi wa madola ya kibepari ya kimagharibi unaoongozwa na Marekani kutokana na chuki zao dhidi ya Uislamu na Waislamu. Wanafikra hao wakifanya utafiti kwa jicho la uadilifu wataukinai ukweli na kuukubali. Na hata lau hawatokubali hilo, basi walau wataweza kuutizama mfumo wa Uislamu kwa heshima, moyo mkunjufu bila ya uadui.

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ
فِي التَّوْرَاةِ وَالْإِنْجِيلِ يَأْمُرُهُمْ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ عَنِ الْمُنْكَرِ
وَيُحِلُّ لَهُمُ الطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ الْخَبَائِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ
وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ فَالَّذِينَ آمَنُوا بِهِ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ
وَاتَّبَعُوا النُّورَ الَّذِي أُنزِلَ مَعَهُ أُوْلَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ (الأعراف:
.(157

"Wale wanaomfuata Mtume, Nabii asiyesoma wala kuandika, wanayemkuta kaandikwa kwao katika Taurat na Injili, anawaamrisha mema na kuwakataza mabaya, na anawahalilishia vizuri, na kuwaharamishia maovu, na anawaondelea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao. Basi wale waliomuamini yeye, na wakamuheshimu, na wakamsaidia, na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye, hao ndio wenye kufanikiwa." (TMQ 7: 157)

******

**MAULID NI MAJUKUMU SIO SHEREHE**

**#MazaziYaMtumeUkomboziKwaGaza**
**#MichagoYaMaulidTupelekeGaza**

## Matukio … kutoka uk 3

bin Ashraf aliyekuwa akimtukana SAAW na Uislamu. Jukumu hili alipewa Muhammad bin Maslamah akiongoza wenzake watatu. Walifanikiwa kukileta kichwa cha Kaab kwa SAAW. (Mwaka wa 3 AH)

7.Vita vya Hamr al- Assad Mara baada ya Vita vya Uhud, katika hali ya kuonyesha kwamba dola haikudhoofika Mtume SAAW alipopata taarifa ya uwezekano wa mushrikuuna kurejea katika uwanja wa vita wa Uhud alitoka na Masahaba wake kuwafukuza asubuhi iliyofuata baada ya Vita vya Uhud (Mwaka wa 3AH.)

8.Ghazwat Banu -Nadhiir. Baada ya mayahudi wa kabila hili kufanya uadui, khiyana na kutaka kumuuuwa

Mtume SAAW walipewa siku 10 waondoke au watauwawa. Wakazingirwa, na wakaruhusiwa baadhi yao kubakia kwa masharti maalum. Ali bin Abi Twalib alikabidhiwa bendera ya vita. Ibn Umm Makhtoum akaongoza Madina kwa muda. (Mwaka wa 4 AH)

9. Ghazwatu-Doumat Al- Jandal.

Mtume SAAW aliongooza kikosi cha askari 1000 kupambana na makabila ya Doumat Jandal yaliokuwa yakipora bidhaa za misafara ambao pia walikusudia kuivamia Madina. Uongozi wa Madina ulikabidhiwa Sibai bin Arfatah Al-Ghifary (Mwaka wa 5AH.)

10.Ghazwatu Banu Lihyan.

**Inaendelea uk 8**

# DINI MSETO HAINA NAFASI KATIKA UISLAMU

**Mwezi Julai 2025,** jumba jipya la ibada katika Kanisa la Arise and Shine Tanzania lililopo Kawe, viungani mwa jiji la Dar es Salaam lilizinduliwa.

Kanisa hilo linaongozwa na Mwinjilisti na anayejiita 'Mtume' Boniface Mwamposa ambaye mahubiri yake mwaka 2020 yalileta msiba wa vifo vya waumini zaidi ya 20 kutokana na mkanyagano waliokuwa wakikimbia kupakwa mafuta yenye baraka.

Sherehe za uzinduzi huo zilitumika kuimarisha maadili ya kidemokrasia na kisekula kwa kusisitizwa na Rais Samia kuhusu umuhimu wa kudumisha mshikamano wa kitaifa na kuwataka Watanzania kulinda amani na umoja wa muda mrefu nchini wakati taifa linapojiandaa kwa Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025.

Fauka ya hayo, hafla kama hiyo ilitumika kuunganisha ajenda hatari sana ya imani mseto kufikia kiwango ambacho vitendo kadhaa vinavyowakilisha kampeni hiyo ya kishetani vilitekelezwa na kusisitizwa mno.

Ilishuhudiwa wakati wa hafla hiyo kuwa baadhi ya viongozi wa Waislamu, wanasiasa wenye asili ya Kiislamu pamoja na Waislamu wa kawaida wakifanya maombi pamoja na wasiokuwa Waislamu ndani ya kanisa hilo, baadhi yao hata wakitoa kauli kinyume na mafundisho na fikra za Kiislamu

Uzinduzi huo ulicheza dori kubwa na ulitumika sana kama jukwaa la kuhubiri na kulingania mazungumzo ya dini mseto kati ya Uislamu na




Ukristo kwa jina la mshikamano wa kijamii au kidini nchini.

Baada ya kufeli kwa Wamagharibi kuwatenga Waislamu na imani (itikadi) yao kupitia wamishenari, orientalisti, kazi za kithaqafa, vyombo vya habari, udanganyifu wa kifikra na wa kisiasa, walitumia njia za mazungumzo ya dini mseto ambayo yalianzishwa rasmi mwaka 1932 na Ufaransa kupitia kutuma ujumbe wake katika Chuo Kikuu cha Azhar.

Lengo lao kuu la kampeni ya mazungumzo ya dini mseto ambayo inasukumwa na dola za kibepari ni kuzuia Uislamu kurudi katika mambo ya maisha kama mfumo mpana. Kwani Uislamu unatishia uhai wa mfumo wao na hadhara yao ya kibepari na kuangamiza maslahi na ushawishi wao.

Kupitia mazungumzo ya dini mseto, mabepari wa Magharibi wanafanya kazi ya kuondoa thaqafa ya Kiislamu katika akili za Waislamu. Wanalenga kufikia hilo kwa kuhujumu imani ya Waislamu kwa thaqafa yao, machimbuko na kanuni zake.

Pia, kampeni hiyo ilimaanisha kuzimua na kudhoofisha mafundisho ya Kiislamu ya nguvu zake za kimaumbile katika kupingana na fahamu za hadhara zisizo za Kiislamu. Bila kutaja njama ya kimagharibi ya kuuvua sifa zake muhimu zaidi zinazoutofautisha na dini nyenginezo, nazo ni za kijamii, kiuchumi na muhimu zaidi nyanja ya kisiasa ambayo kwayo Khilafah ndiyo dola yake.

Waislamu nchini Tanzania na kwengineko wanapaswa kuwa waangalifu na ajenda hii ovu ya kimataifa inayoendelea ya mazungumzo baina ya dini mseto, kwa upande wa fikra na vitendo.

Ijapokuwa Uislamu unaruhusu ushirikiano wa kisheria na wasiokuwa Waislamu, lakini hiyo haipanuki hadi kwenye mshikamano wa kidini, na unakataza kabisa ushiriki wowote katika matendo yoyote ya ibada ya dini nyengine. Dini pekee ya haki ni Uislamu, ambayo Waislamu wanapaswa kujishughulisha katika dawah ili kanuni zake zote zitabikishwe chini ya dola yake ya Khilafah.

********

## Matukio … kutoka uk 7

Mtume SAAW aliongoza kikosi cha watu 200 kwenda kulipiza kisasi cha kuuliwa mas'haba wake katika tukio la Arrajii. Ibn Ummu Makhtoum aliteuliwa kushikilia madaraka ya dola kwa muda. (Tukio hili ama lilitokea Rabi-ul Awwal au Jamadul- thanii Mwaka wa 6AH)

11. Kutumwa kikosi cha Ukasha bin Mihswam
Kikosi hiki kilitumwa Al-Ghamr kwa Bani Assad.Makafiri walikimbia, na Waislamu wakapata ngawira ya ngamia 200 (Mwaka wa 6 AH.)